
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Taarifa ya ALMA ya Robo Mwaka**
**Robo ya Pili, 2026**

**MUUNGANO WA VIONGOZI WA AFRIKA KATIKA KUDHIBITI MALARIA**

# Kadi ya Alama ya Uwajibikaji na Utekelezaji

Ramani inayoonesha mtawanyo wa ugonjwa wa malaria kutokana na mbu aina ya *Plasmodium falciparum* mwaka 2020, nchini Tanzania




**Vipimo**

| | | |
|---|---|---|
| **Sera** | | |
| Kusaini, Kuidhinisha na kuwasilisha Mkataba wa AMA AUC | | |
| Uwepo wa Mikakati inayolega kambi za wakimbizi kwenye mpango mkakati wa malaria | | |
| Uwepo Uwepo wa Mikakati inayolega watu wa ndani ya nchi wasio na makazi maalum kwenye mpango mkakati wa malaria | | |
| Nchi inatoa taarifa za uzinduzi wa Kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na mimi | | |
| Uzinduzi wa Baraza la Kutokomeza Malaria | | |
| Utambulisho wa chanjo ya Malaria | | |
| **Ufuatiliaji wa Usugu, Utekelezaji na Matokeo yake** | | |
| Tafiti za kufuatilia ufanisi wa dawa za kutibu malaria umefanyika tangu mwaka 2019 na taarifa zake kutumwa Shirika la Afya Duniani | | |
| Ufuatiliaji wa usugu wa mbu dhidi ya viuatilifu tangu 2020 na taarifa kuripotiwa kwa Shirika la Afya Duniani | | |
| % ya Vyandarua / Viuatilifu Ukoko vilivyopokewa nchi mwaka jana ikijumuisha viuatilifu vipya | | 84 |
| Akiba ya dawa mseto (ACTs) (Ya zaidi ya miezi 6) | ▲ | |
| Akiba ya vitendanishi (RDTs) (Ya zaidi ya miezi 6) | | |
| Kupungua kwa Idadi ya Visa vipya kwa asilimia 75 au zaidi kwa mwaka 2025 (ukilinganisha na takwimu za 2015) | | |
| Kupungua kwa idadi ya Vifo kwa asilimia 75 au zaidi kwa mwaka 2025 (ukilinganisha na takwimu za mwaka 2015) | | |
| **Viashiria vya Afya ya uzazi, afya ya mtoto na UVIKO 19** | | |
| Idadi waliofikiwa na umezeshaji wa dawa za kinga tiba dhidi Magonjwa ya Tropiki yaliyosahaulika kwenye jamii (NTD index, %)(2024) | | 73 |
| % ya ugawaji dawa kwa walengwa ili kufikia Malengo ya Shirika la Afya Duniani | | 60 |
| Bajeti ya Serikali iliyotengwa kwa ajili ya magonjwa ya kitropiki ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele | | |
| Makadirio ya asilimia ya watoto, kati ya miaka 0-14, waishio na VVU ambao wanapata dawa za ARV (2025) | | 70 |
| Kiwango cha chanjo ya DPT3 2025 (miongoni mwa watoto wenye miezi 0-11) | | 83 |
| Mabadiliko ya tabia nchi Magonjwa yanayoenezwa na wadudu na michango iliyoamuliwa kitaifa | | |

Malaria imeenea katika maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukiwa na ongezeko kubwa (vilele) katika msimu. Taarifa ya malaria ya mwaka 2024 imeonesha idadi ya wagonjwa ilikuwa 3,586,513 na vifo 1,533 vinavyotokana na Malaria.

## Ufunguo:

- Lengo limefikiwa/utekelezaji unaenda vizuri
- Kuna mafanikio lakini juhudi zaidi zinahitajika
- Utekelezaji upo nje ya lengo
- Hamna Takwimu
- Haihusiki

## Malaria – Msukumo Mkubwa Kuelekea Mwaka 2030

Bara la Afrika liko katikati ya dhoruba kali linalotishia kuvuruga utoaji huduma na kuathiri maendeleo yaliyopatikana katika udhibiti wa malaria kwa karne zilizopita. Ni lazima nchi kuchukua hatua za haraka kuzuia na kupunguza athari mbaya kufuatia mgogoro wa kifedha unaoendelea duniani, kupungua kwa misaada ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea - ODA, kuongezeka kwa tishio la kibailojia, mabadiliko ya hali ya hewa na madhara ya kibinadamu. Matukio haya yanatishia sana kuvuruga mafanikio yaliyopatikana katika udhibiti wa malaria kwa takriban miaka 20, na huenda yakasababisha ongezeko la majanga na milipuko ya magonjwa, iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa. Ili kuwa na mwendelezo sahihi na hatimae kutokomeza kabisa malaria, tutahitaji kukusanya dola za kimarekani bilioni 5.2 kila mwaka, ili kufadhili kikamilifu mahitaji ya mipango yetu ya kitaifa ya malaria, na kwa uharaka kujaza mapengo yaliyotokana na kupungua hivi karibuni kwa misaada ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea.

Matukio ya hali ya hewa kali na mabadiliko ya hali ya hewa ni tishio kubwa kwa maendeleo yaliyopatikana. Hadi kufikia mwaka 2030, watu milioni 150 zaidi watakuwa katika hatari ya kuugua malaria kwa sababu ya ongezeko la joto na kuongezeka kwa mvua. Ni lazima nchi kuchukua hatua ya kukabiliana na matishio ya usugu wa viuatilifu na usugu wa dawa za kutibu malaria, kupungua kwa ufanisi wa vipimo vya uchunguzi vinavyotoa majibu kwa haraka, na uwepo wa mbu vamizi aina ya *Anofelesi Stephensi* ambae anaeneza malaria katika maeneo ya mjini na vijijini. Zana za udhibiti wa malaria zinaendelea kuongezeka.

Shirika la Afya Duniani limeidhinisha matumizi ya vyandarua vipya venye aina mbili za viuatilifu ambavyo vina ufanisi kwa asilimia 43 zaidi, ukilinganisha na vyandarua vya kawaida na matumizi ya vyandarua hivi vipya yatasaidia sana katika kudhibiti athari za usugu wa viuatilifu. Shirika la Afya Duniani pia limeidhinisha matumizi ya dawa ya kupulizia angani. Dawa mpya za kutibu malaria na chanjo aina mbili za malaria kwa ajili ya watoto, tayari zimepitishwa na kuna ongezeko la nchi kadhaa za Afrika, ambazo zimeanza kutumia zana hizo mpya za udhibiti wa malaria. Malaria imekuwa mfano wa kuonesha njia katika uimarishaji wa huduma za afya ya msingi, mabadiliko ya hali ya hewa, afya, na Huduma ya Afya kwa Wote.

Nchi zinatakiwa kuongeza uwekezaji wa rasilimali toka vyanzo vya ndani ya nchi ikijumuisha ushirikishwaji wa sekta mbalimbali katika Mabaraza na fedha za kutokomeza malaria na magonjwa ya kitropiki ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele, ambapo mpaka sasa zimekusanywa zaidi ya dola za kimarekani milioni 245.

Taarifa ya hivi karibuni kutoka Muungano wa Viongozi wa Afrika katika Kudhibiti Malaria – ALMA, na Taasisi ya "Hamna Tena Malaria" ya Uingereza, zinaonesha athari ya "Gharama ya Kurudi Nyuma" zinazotokana na Malaria kati ya mwaka 2025 na 2030, kwenye Pato la Taifa, biashara na sekta muhimu kwa maendeleo barani Afrika. Iwapo Tanzania haiwezi kuendeleza udhibiti wa malaria kutokana

na kupungua kwa ufadhili, itasababisha ongezeko la wagonjwa wa ziada karibia 22,189,017, kiwango cha mvua na vifo vya ziada 65,656 na upotevu katika Pato la Taifa wa dola za kimarekani bilioni 3.5 kati ya mwaka 2025 na 2030. Hata hivyo, iwapo tutakusanya rasilimali muhimu na kufanikiwa punguza Malaria kwa asilimia 90, Tanzania kutakuwa na ongezeko la dola za kimarekani bilioni 7.7 katika Pato la Taifa.

**Hatua iliyofikiwa.**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya ufuatiliaji usugu wa viuatilifu tangu mwaka 2015 na imekuwa ikitoa taarifa ya matokeo kwa Shirika la Afya Duniani, na imesaidia kukabiliana na viwango vilivyobainika vya usugu katika kufanya maamuzi ya kuongeza vyandarua vipya vya kizazi kijacho vyenye ufanisi mkubwa. Nchi pia imefanya ufuatiliaji wa usugu wa dawa tangu mwaka 2018 na imekuwa ikitoa taarifa ya matokeo ya usugu wa dawa kwa Shirika la Afya Duniani. Mpango mkakati wa kitaifa unajumuisha shughuli zinazolenga wakimbizi. Aidha nchi tayari imezindua kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na Mimi.

Sambamba na ajenda ya kipaumbele ya Mwenyekiti wa ALMA, Rais Wakili Duma Gideon Boko, nchi imeimarisha mifumo ya ufuatiliaji na uwajibikaji kwa ugonjwa wa Malaria kwa kutengeneza Kadi ya Alama ya Kudhibiti na Kutokomeza Malaria, ingawa Kadi ya Alama bado haijashirikiwa kwenye Kituo cha Kadi ya Alama cha ALMA. Nchi imezindua Baraza na Mfuko wa kutokomeza kabisa Malaria.

## Matokeo:

Taarifa ya mwaka 2024, inaonesha kuwa idadi ya wagonjwa wa Malaria ilikuwa 3,586,513 na idadi ya vifo vilivyotokana na Malaria vilikuwa 1,533.

## Changamoto Kuu:

- Kudumisha Malaria kuwa ajenda muhimu yenye utashi wa kisiasa na kutenga fedha kwa ajili ya Zanzibar, hasa ikizingatiwa kuwa maambukizi ya Malaria visiwani humo yanaendelea kupungua.

- Rasilimali zisizotosheleza katika kutekeleza kikamilifu Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Malaria ikijumuisha athari za hivi karibuni za kupunguzwa kwa misaada ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea - ODA.

- Tishio la uwepo wa usugu wa viuatilifu na usugu wa dawa za kutibu Malaria.

## Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyopita:

| Lengo | Vipengele vya Utekelezaji | Muda wa Kukamilisha Utekelezaji | Hatua ya Utekelezaji | Ufafanuzi wa shughuli/ mafanikio ukilinganisha na taarifa ya utekelezaji wa robo iliyotangulia |
|---|---|---|---|---|
| Matokeo | Kufanyia kazi ili kuhakikisha mikakati ya kutokomeza malaria inapewa kipaumbele katika Mkataba wa Maelewano wa Kwanza unaohusu Mkakati wa Afya wa Marekani na kuhakikisha inaandaliwa mipango ya kipaumbele yenye makadirio ya gharama. | Robo ya 1 2026 | | Tanzania tayari imesaini Mkataba wa Maelewano na Serikali ya Marekani. |

# Huduma ya Afya ya Uzazi kwa Mama, Mtoto Mchanga, Mtoto na Vijana:

## Hatua iliyofikiwa.

Tanzania imefanikiwa kufikia kiwango cha juu katika kiashiria cha Huduma ya Afya ya Uzazi kwa Mama, Mtoto Mchanga, Watoto na Vijana katika ugawaji wa vidonge vya Vitamini A na Chanjo ya DPT3 kwa jamii. Tanzania imeimarisha sana mifumo ya ufuatiliaji na uwajibikaji kwa kuandaa na kuzindua Kadi ya Alama yenye Takwimu za Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto Mchanga, Watoto na Vijana, pamoja na utayarishaji wa Kadi ya Alama ya Masuala ya Lishe kwa Sekta mbalimbali.

# Magonjwa ya Kitropiki ambayo Yalikuwa Hayapewi Kipaumbele:

## Hatua iliyofikiwa.

Mafanikio ya kudhibiti Magonjwa ya Tropiki ambayo Yalikuwa Hayapewi Kipaumbele, kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yanapimwa kwa kutumia fahirisi ya kielezo kinachozingatia kiwango cha utekelezaji wa dawa-kinga kwa Magonjwa ya matende, usubi, kichocho, minyoo na trakoma. Mwaka 2024, kiwango cha utekelezaji wa dawa-kinga kilikuwa asilimia 63 kwa udhibiti wa Minyoo, asilimia 68 kwa kichocho, asilimia 69 kwa udhibiti wa matende, asilimia 86 kwa udhibiti wa usubi, na asilimia 83 kwa trakoma.

Kiwango cha ujumla cha utekelezaji kwa Magonjwa ya Tropiki ambayo Yalikuwa Hayapewi Kipaumbele kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2024 ni alama 73 ikionesha mafanikio makubwa ukilinganisha na mwaka 2023 ambapo alama ilikuwa (39). Nchi haikufikia malengo ya Shirika la Afya Duniani katika ugawaji wa dawa-tiba kwa kichocho na minyoo kwa mwaka 2024 pekee. Tanzania imeweka kifungu maalum katika bajeti kwa ajili ya Magonjwa ya Kitropiki ambayo Yalikuwa Hayapewi Kipaumbele.

### Ufunguo:

| | |
|---|---|
| | Utekelezaji umekamilika |
| | Utekelezaji umefanyika kwa kiasi |
| | Hamna utekelezaji |
| | Muda wa kutekeleza haujafika |